



THE REPUBLIC OF UGANDA
MINISTRY OF HEALTH

MPOX

UNACHOHITAJI KUJUA

Mpox (hapo awali iliitwa Monkeypox) ni ugonjwa wa zoonotiki wa virusi (virusi vinavyopitishwa kwa wanadamu kutoka kwa wanyama) ambao hutokea hasa katika maeneo ya misitu ya kitropiki ya Afrika ya kati na magharibi na mara kwa mara husafirishwa hadi mikoza mingine.

Mpox husababishwa na virusi. Dalili zake ni kama zile zinazoonekana kwa wagonjwa wa ndui, ingawa si kali sana.

Ishara na dalili:

- Upele wa ngozi
- Homa
- Vidonda vya kooni
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya mwili
- Maumivu ya mgongo
- Nguvu chache
- Kuvimba kwa nodi za limfu



Unaeneaje?

- Kugusana kwa mwili wa mtu na wa mwengine:
 - Kugusa kwa karibu na vidonda vya ngozi na maji ya mwili.
 - Kuvuta chembechembe za pumzi zilizochafuliwa au virusi.
 - Njia iliyotipotiwa zaidi ya maambukizi ni ngono.
 - Nyenzo zilizochafuliwa k.m sindano, michoro ya kimwili matandiko, vitambaa, nguo, vyombo vya kulia na vinyago vya ngono, miongoni mwa vingine.
- Mpox huambukizwa kwa binadamu kwa kuwasiliana kwa karibu na aliyeambukizwa au mnyama au kwa nyenzo zilizoambukizwa.

Ni nani yuko kwenye hatari ya kuambukizwa Mpox?

Watu walio katika maingiliano ya karibu na wagonjwa wa Mpox, k.m wanafamilia na washirika wa ngono (ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wa ngono ya biashara).

Watu wanaohudumia wagonjwa wa Mpox bila matumizi sahihi ya vifaa vya kinga binafsi.

Watu ambao huwinda, kuua, kushughulikia, kuchinja na kuandaa wanyama kama vile kuke, panya na nyani.

Watu wanaofanya kazi katika maabara bila matumizi sahihi ya vifaa vya kinga binafsi.

Watoto, wajawazito, na wale ambao wanaweza kuwa dhaifu kwa sababu ya hali nyingine za kiafya

Watu ambao wana wapenzi wengi na/au wenzi wa ngono wa mara kwa mara wasiojulikana

Ingawa baadhi ya watu wanaweza kuwa katika hatari zaidi kuliko wengine, ni muhimu kukumbuka kwamba mtu yeyote, popote, anaweza kupata Mpox

Kwa habari zaidi, wasiliana kwa laini ya simu ya bure ya Wizara ya Afya: 0800100066 au tuma UJUMBE MFUPI kwa U-Report kwa 8500

Unajikinga vipi na maambukizi?

- Epuka ukaribu (uso kwa uso, ngozi kwa ngozi, mdomo-kwa-ngozi, na mdomo-kwa-mdomo) na watu ambao wamethibitishwa kuwa nao Mpox au walio na dalili za Mpox.
- Epuka kugusa au kutumia kwa pamoja vitu vya kibinafsi kama matandiko, vyombo vya kulia chakula, nguo, simu au vitu vingine vya mtu aliye ishara na dalili za Mpox.
- Epuka kuwasiliana na wanyama wote wa porini (hai au waliokufa), hasa wale wanaojulikana kubeba virusi kama vile panya au nyani, na wale wanaoonekana wagonjwa au wamekutwa wamekufa.
- Epuka kula wanyama wa porini (kuke, panya na nyani)
- Chanjo ya ndui inaweza kutolewa kwa watu wanaogusana kwa karibu na watu walioambukizwa au walio katika harakati kubwa ya kuambukizwa.